# UJANA SALAMA: MUUNDO WA ZIADA YA PESA (CASH PLUS) KUHUSU USTAWI NA MABADILIKO SALAMA YENYE AFYA KWA VIJANA

Matokeo ya Kati Mei, 2019

THE TRANSFER PROJECT





© UNICEF/UNI94708/Noorani

## UTANGULIZI

Ufupisho huu unawasilisha matokeo ya kati ya mradi wa Cash Plus uliotekelezwa Tanzania vijijini na Tanzania Social Action Fund (TASAF). Mradi huu wa majaribio, unaojulikana kama "Ujana Salama" unaendeshwa na kutekelezwa na taasisi ya serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania ya mtandao wa kijamii wa uzalishaji salama (PSSN), wakisaidiwa kiufundi na Shirika la Kimataifa la kuhudumia Watoto - UNICEF Tanzania na tume ya kupambana na UKIMWI Tanzania (TACAIDS). Mradi wa Ujana Salama, unalenga vijana wadogo katika kaya zinazopokea PSSN (inayojumuisha ruzuku, mpango wa ajira za muda, na mipango ya kuweka akiba na kuwekeza) na ulioundwa kuendana na kitengo cha PSSN cha mipango ya kuweka akiba na kuwekeza.

Vijana wadogo walio Tanzania vijijini wanakabiliana na changamoto nyingi za kiafya na kiuchumi, hata kwa wale vijana wadogo wanaoishi katika kaya zinazofaidika na mradi wa PSSN. Kinga ya jamii inaendelea kuonekana kama nyenzo muhimu ya uwekezaji kwa vijana wadogo ili kuhakikisha wanaendelea kuwa na afya, na kuwa watu wazima wazalishaji. Kuwekeza kwa vijana wadogo kuna manufaa yenye tija katika kupunguza umaskini na kukuza uchumi ikizingatiwa vigezo vingine vinavyoendana kama uwekezaji katika miundombinu na kutengeneza mazingira wezeshi kwa uzalishaji wa kazi. Mradi wa Cash Plus unahamishwa na ushahidi kwamba kinga ya jamii katika muundo wa ruzuku inaweza kuwa na ushawishi chanya kwa ustawi wa vijana. Hata hivyo huwa ni nadra kutosheleza kushinda hatari zinazohusiana na ujana. Kama ilivyoainishwa katika ripoti ya awali ya Cash Plus, vijana katika kaya za PSSN bado wanakabiliwa na changamoto lukuki kama kuacha shule, mimba za utotoni, magonjwa ya ngono pamoja na UKIMWI, ukatili, manyanyaso na unyonyaji. Ukosefu wa fursa za kiuchumi unazuia mabadiliko salama kuelekea utu uzima kwa vijana wadogo. Kukabiliana na changamoto hizo, mradi wa Cash Plus umetumia matokeo ya PSSN pamoja na miradi ya ziada kama vile mafunzo na kuunganisha na huduma, kujibu udhaifu maalum kwa vijana wadogo. Lengo la mwisho la mradi huu ni kuwezesha mabadiliko salama, yenye afya na yenye tija kuelekea utu uzima. Mradi huu pia una lenga kujenga na kustawisha uwezo wa serikali za mitaa na huduma zinazohusiana na afya, mpango wa kuweka akiba na kuwekeza na kinga ya jamii kwa vijana wadogo.

## UJANA SALAMA: MRADI WA CASH PLUS

Ukipangiliwa juu ya PSSN inayoendelea, Ujana Salama unajumuisha nyanja tatu 1) stadi za maisha na elimu juu ya afya ya ngono na uzazi na VVU na stadi za maisha, 2) kuboresha upande wa usambazaji kwa kuwaunganisha vijana wadogo na huduma rafiki za afya kwa vijana zinazohusiana na VVU/UKIMWI, afya ya ngono na uzazi na kukabiliana na ukatili 3) maelekezo baada ya mafunzo na uhamisho wa mali, ambapo vijana wadogo wanaunganishwa na waelekezaji wanaowafundisha kuhusu machaguo ya mipango ya kuweka

The Transfer Project
transfer@unc.edu
https://transfer.cpc.unc.edu/

EDI Group
A MATHEMATICA COMPANY
unicef

akiba na kuwekeza na matatizo ya maisha na kupokea mpango wa ajira za muda ili kuweza kutimiza elimu yao, stadi za maisha au mipango ya biashara. Mamlaka za eneo la utekelezaji (PAA) mbili zilichaguliwa kutekeleza mradi wa Ujana Salama, kufuatana na kuingiliana kati ya vipaumbele vya TASAF na mikoa ambayo UNICEF ilikuwa tayari inasaidia miradi inayoendelea. Ikama hii inatekelezwa katika wilaya nne za kusini mwa Tanzania: Mufindi/Mafinga huko Iringa na Rungwe/Busokelo huko Mbeya. Mafunzo ya uso kwa uso kwa vijana wadogo yalifanyika katika kipindi cha wiki 12 kati ka mwezi Februari na mwezi Mei 2018. Wawezeshaji walikutana na vikundi vya vijana katika kila kijiji kwa saa mbili mpaka nne, mara moja kwa wiki, kwa muda wa wiki kumi. Mafunzo hayo yalitanguliwa na wiki ya ufunguzi na ya ufungaji. Mafunzo ya mipango ya kuweka akiba na kuwekeza na UKIMWI na afya ya uzazi na ngono yalifanyika kwa pamoja katika kila kipindi (saa moja mpaka mbili kwa kila kimojawapo) na yalijumuisha masomo yafuatayo:

*Umbo 1: Masomo* makuu ya mafunzo

*Mipango ya kuweka akiba na kuwekeza*

- Ndoto na malengo
- Mbinu za ujasiriamali
- Mipango ya biashara na utunzaji kumbukumbu
- Utunzaji wa akiba

*VVU na Afya ya ngono*

- Kukabiliana na balehe
- Mahusiano
- Elimu ya VVU, kinga na kujilinda
- Tabia hatarishi za ngono na kujilinda
- Mimba na uzazi wa mpango
- Ukatili na ukatili wa kijinsia
- Kukabiliana na mitazamo na tamaduni hasi za kijinsia
- Pombe na dawa za kulevya
- Kuishi kiafya na lishe

Maelekezo baada ya mafunzo yanategemewa kuendelea kwa wastani wa miezi tisa, na katika kipindi hicho vijana waliohudhuria mafunzo na wakatengeneza mpango (wa biashara au kuendelea na elimu/stadi za kazi) watapokea ruzuku (kiwango sawa na dola za kiMarekani 80).

## TATHMINI

Ili kuelewa ufanisi wa mradi huu, tathmini ya matokeo inaongozwa na Ofisi ya utafiti ya UNICEF – Innocenti pamoja na shirika la mpango wa maendeleo ya uchumi (EDI) wakishirikiana na TASAF, TACAIDS pamoja na UNICEF Tanzania.

Kupima utekelezaji kwa njia ya takwimu kutatumia muundo wa maeneo linganifu yaani ambayo ina mikono miwili (mkono wa ikama wa waliopokea PSSN + vijana Cash Plus na mkono wa ulinganifu wa wanaopokea PSSN pekee), ambayo inaruhusu watafiti kutathmini matokeo ya kifurushi cha Cash Plus kwa ustawi wa vijana kati ya nyumba za PSSN. Tathmini hii endelevu ni ya miaka miwili, endelevu na ya kutumia mbinu mchanganyiko ikijumuisha tafiti za awali (Aprili – Juni 2017), wa kati (2018) na wa mwisho unaotarajiwa kufanyika mwaka wa 2019. Taarifa za ki-takwimu zilikusanywa kutoka vituo vya afya, jumuiya, viongozi wa kaya na vijana. Pia, mahojiano ya kina yalifanyika kwa jumla ya vijana 32. Tathmini ya kati ilifanyika mara tu baada ya mafunzo ya wiki 12 kuhusu mipango ya kuweka akiba na kuwekeza na stadi za maisha, lakini kabla ya mafunzo elekezi na kupokea ruzuku.

*Umbo la 2: Matokeo muhimu*

Vijana katika pande zote mbili za utafiti walihojiwa katika awamu zote za ukusanyaji taarifa. Awali, wahojiwa walijumuisha vijana 2,458 wa umri wa kati ya miaka 14-19. Kati ya hao, 2,104 walihojiwa tena katika mahojiano ya kati, wakiwakilisha asilimia 86 wa wahojiwa wa kujirudia. Matokeo yanayoelezewa kwenye ufupisho huu yanalenga takwimu kutoka vijana waliohojiwa mara ya awali na ya kati, ambayo hujulikana pia kama "jopo la sampuli". Asilimia ya vijana waliopotea katika ufuatiliaji ni sawa kati ya vijiji vya majaribio na na vile vya ulinganifu, na sifa zao bado zimebakia zikilingana kati ya pande hizo mbili kwa jopo la sampuli.

Kwa uchambuzi wa kitakwimu uliochunguza matokeo au athari katika kipindi cha kati, tulitumia takwimu za awali na za kati toka kwa vijana wa vijiji vya majaribio na vile vya ulinganifu, na tukalinganisha mabadiliko baada ya muda kwa makundi hayo mawili. Kwa uchambuzi wa mahojiano ya kina, tulichunguza njia mbalimbali ambazo mabadiliko yalitokea.

## MATOKEO YA KATI

Kwa kipindi cha kati, tunaona baadhi ya matokeo chanya katika matokeo ya muda mfupi, pamoja na yale yanayohusiana na afya ya ngono na uzazi, taarifa za VVU na mitazamo linganifu ya kijinsia. Matokeo haya yanaonesha jinsi katika kipindi hiki cha majaribio, vijana wadogo wameweza kuanza kupata uelewa na kufikiria kuhusu maisha yao ya baadaye kwa namna mbalimbali. Hata hivyo, kulikuwa na muda mfupi wa kushiriki kwenye majaribio mpaka kipindi cha kati na baadhi ya vipengele vilikuwa bado havijatekelezwa. Pia, matokeo mengine huchukua muda mpaka kuonekana, kwa mfano mabadiliko ya tabia na uzoefu vinaweza kuchukua muda zaidi kuonekana. Kwa sababu hizi, hatuoni katika kipindi hiki cha kati mabadiliko katika matokeo muhimu ya kipindi cha kati na cha muda mrefu kuhusu kuanza ngono, mahusiano, kutafuta huduma za afya na uzoefu wa ukatili.

### *Elimu, kujishughulisha kiuchumi na matarajio*

- Mradi uliongeza ushiriki wa vijana wadogo katika shughuli za kiuchumi. Ongezeko hili lilisukumwa zaidi na ongezeko la ushiriki katika kuchunga mifugo ya familia na pia inawezekana ni matokeo ya vijana kuanza shughuli zao binafsi za ufugaji. Kutoka kwenye mahojiano ya kina, tunaona kwamba vijana wadogo wanaona kuchunga mifugo kama sehemu ya awali ya kuanza kuwa na mali ambazo baadaye zitawekezwa kwenye elimu au biashara nyingine. Hata hivyo, ongezeko la ushiriki wa kuchunga mifugo haukupelekea kuongezeka kwa saa zilizotumiwa katika shughuli za kiuchumi.
- Ushiriki wa vijana wadogo katika shughuli za nyumbani haukuathiriwa na mradi, kasoro ongezeko ya ushiriki katika kuokota kuni.
- Pia, mafunzo ya Cash Plus yalifanyika nje ya muda wa masomo, na hivyo mradi haukusababisha utoro wa shule. Kihalisia, mradi ulikuwa na matokeo ya kuzuia utoro kati ya mabinti walio na umri wa zaidi ya miaka 16.
- Mradi haukuwa na madhara kwa matarajio ya kielimu.
- Mradi pia uliongeza kiwango cha vijana wanaotaka kuwa wamiliki wa biashara.

*Muda– mfupi:* matarajio ya kielimu na kiajira; mitazamo linganifu ya kijinsia; ujuzi wa njia za kisasa za uzazi wa mpango, ujuzi kuhusu kujikinga na VVU; na ujuzi wa sehemu za kupata huduma za afya ya uzazi na ngono na kupata msaada wa ukatili.

*Kati na muda mrefu:* nafasi za ajira kwa vijana na mbinu za kuingiza kipato; kupata elimu na mafunzo; kuongeza uwezo wa kupata huduma sahihi za afya ya uzazi na ngono, ndoa na mimba; kupunguza kujihusisha na mahusiano ya kingono ya kinyanyasaji, tabia hatarishi za kingono; hali nafuu ya afya ya akili; kupungua kwa ukatili na unyanyasaji.

### *VVU, afya ya ngono na uzazi na kuunganishwa kwenye huduma*

- Mradi uliongeza ujuzi wa kujikinga na VVU kati ya mabinti, lakini sio kwa vijana wa kiume. Mradi uliongeza ujuzi wa mabinti kwamba kufanya ngono na mpenzi mmoja, asiye ambukizwa inaweza kupunguza hatari ya VVU. Kama ambavyo vijana wa kiume kwa ujumla, wana ujuzi zaidi wa VVU na afya ya uzazi na ngono, matokeo yetu yanaamanisha kwamba mradi unasaidia mabinti waweze kuwakaribia wavulana.
- Katika ujuzi mwingine unaohusiana na viashiria vya VVU (kama mbu au chakula vinaambukiza VVU kwa mfano), kulikuwa na taarifa sahihi za juu hapo awali (zaidi ya asilimia 90) na hivyo kulikuwa na nafasi ndogo ya maboresho kama matokeo ya mradi. Hasa, hakukuwa na matokeo katika viashiria hivi wala ujuzi kwamba matumizi ya mipira ya kondom ya mara kwa mara, yanazuia hatari ya VVU.



- Mradi uliongeza ujuzi wa njia moja au zaidi ya kisasa ya uzazi wa mpango. Tena, matokeo yanaendeshwa na washiriki wa kike. Zaidi, kama matokeo ya ikama, vijana walikuwa na uwezekano mdogo zaidi kutoa taarifa kwamba hawafahamu kuhusu njia za uzazi wa mpango au mipira ya kondom (matokeo muhimu yakionekana kwa mabinti kuliko wavulana).
- Hakukuwa na ongezeko katika idadi ya vijana wadogo waliotafuta huduma za afya ya uzazi na ngono au kupima VVU au tiba. Hata hivyo, kati ya wale wanaotafuta huduma, kulikuwa na mabadiliko katika aina ya huduma walizotafuta, vijana wadogo walioshiriki katika mradi walikuwa na uwezekano zaidi wa kutafuta huduma za kinga na kuliko kutafuta huduma zinazohusiana na mimba, kulinganisha na vijana wa upande wa ulinganifu.
- Huduma za afya zinaendelewa kuwa rafiki kadri muda unavyokwenda, japo matokeo hayakuonekana kwenye mada zilizozungumzwa au kuona ubora wa afya kama matokeo ya ikama.
- Pia hakukuwa na matokeo kwenye taarifa za kujenga mahusiano, kuanza ngono na sifa za kuanza tendo la kwanza la ngono; uzazi au matumizi ya kinga za mimba, ngono ya kubadilishana au hisia za hatari ya VVU au kupima.

*Usawa wa kijinsia, kupunguza ukatili, afya ya akili na mitazamo*

- Ikama ya Cash Plus iliongeza mitazamo ya usawa wa kijinsia kati ya wavulana (lakini sio wasichana), hasa katika kipengele cha ukatili na shughuli za nyumbani.
- Mpaka kipindi cha kati, ikama haikuwa na matokeo katika uzoefu wa ukatili kwa vijana wadogo wa kihisia, kimwili wala kingono.
- Kuhusu afya ya akili, hakukuwa na matokeo ya kuonesha dalili za sonona au kuhisi shida.
- Mradi haukuwa na matokeo kwenye kuridhika na maisha, kujiamini, kujitawala, ujasiriamali au msaada wa kijamii.

## HITIMISHO

Hivyo, mradi wa Cash Plus uliofanyiwa tathmini hapa, unalenga kutumia matokeo ya Cash Plus kwa kuwapatia vijana mafunzo ya ziada ya mipango ya kuweka akiba na kuwekeza na afya ya uzazi na ngono na VVU, usimamizi na ruzuku na pia kuwezesha kuunganishwa na huduma Rafiki kwa vijana za afya ya uzazi na ngono na VVU.

Matokeo ya kati yameonesha matokeo chanya ya mradi katika VVU na ujuzi wa VVU na avya ya uzazi na ngono, pia umeongeza mitazamo ya haki ya jinsia na pia matarajio kuwa vitendo. Hasa, mabadiliko ya kitabia huchukua muda zaidi kuonekana.

Matokeo ya utafiti huu yatatupatia taarifa za muhimu kuhusu ubora wa ikama ya Cash Plus iliyofanyika ndani ya shughuli za Serikali za kinga ya jamii, na pia yatachangia kwenye uelewa wa jinsi mbinu za ziada ndani ya mradi wa ruzuku wa Serikali zinavyoweza kuchangia mabadiliko salama ya vijana wa kiTanzania, Afrika kusini mwa Sahara na pia duniani.

Fedha za majaribio haya na tathmini zimetolewa kwa ukarimu wa shirika la Oak Foundation na UNICEF Tanzania. Fedha za ziada kwa ajili ya tathmini zilitolewa na mashirika ya DFID na SIDA, kwa pamoja kupitia ruzuku kwa UNICEF Office of Research – Innocenti kusaidia mradi wa Transfer. Pia, fedha za ziada kwa ajili ya shughuli za utekelezaji zilitolewa na shirika la Irish Aid.

Kwa taarifa zaidi kuhusu mradi na matokeo ya kipindi cha kati, tafadhali angalia ripoti kamili (inapatikana mtandaoni katika tovuti ya https://transfer.cpc.unc.edu/tools/reports/tanzania-reports-2/): Timu ya Tathmini ya Tanzania Cash Plus (2019). Tathmini ya matokeo: Ripoti ya kipindi cha kati. Ofisi ya Utafiti ya UNICEF na EDI. Florence, Italia/ Dar es Salaam, Tanzania.

1 Handa, S., Halpern, C. T., Pettifor, A., & Thirumurthy, H. (2014). The government of Kenya's cash transfer program reduces the risk of sexual debut among young people age 15-25. *PLoS One*, 9(1), e85473-e85473. Heinrich, C. J., Hoddinott, J., & Samson, M. (2017). Reducing adolescent risky behaviors in a high-risk context: The effects of unconditional cash transfers in South Africa. *Economic development and cultural change*, 65(4), 619-652.

2 Watson, C., & Palermo, T. (2016). Options for a "Cash Plus" Intervention to Enhance Adolescent Well-being in Tanzania: An introduction and review of the evidence from different programme models in Eastern and Southern Africa.

3 For administrative purposes, TASAF refers to geographic areas of program implementation as Project Authority Areas (PAAs). On the mainland, these are the same as local government councils. Then, within PAAs there are wards, and within wards, villages/mitaas (a mtaa is an urban administrative unit in urban areas, equivalent to a village in rural areas).

4 We use an Analysis of Covariance (ANCOVA) specification, where we control for the baseline value of the considered outcome.